*Tangazo la Serikali a. 346 (linaendelea)*

TANGAZO LA SERIKALI NA.. 346 la tarehe 28/8/2015

HERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa Chini ya kifungu cha 153)*

IERIA NDOGO ZA (KILIMO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MEATU ZA MWAKA, 2015

| | | |
|---|---|---|
| Jina na Mwanzo wa kutumika. | 1 | Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Kilimo) za Halmashauri ya Wilaya ya Meatu za mwaka 2015 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. |
| Eneo la Matumizi | 2 | Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Meatu. |
| Tafsiri | 3 | Katika Sheria ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelekezwa vinginevyo:- |

*"Afisa mwenye mamlaka"* Maana yake ni Afisa aliyeteuliwa na Halmashauri kwa mujibu wa sheria Ndogo hizi.

*"Halmashauri"* maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Meatu.

*"Kanda za kilimo"* maana yake ni sehemu mbalimbali zinazofaa kwa kilimo cha mazao mbalimbali kama zilivyoonyeshwa kwenye jedwali la kwanza la sheria ndogo hizi.

*"Mazao"* maana yake ni mimea yoyote iliyopandwa na kutunzwa kwa lengo la

matumizi mbalimbali ya binadamu.

*"Mazao ya biashara"* maana yake ni mazao yaliyotajwa kwenye jedwali la pili la sheria ndogo hizi.

*"Mazao ya chakula"* maana yake ni mazao yaliyotajwa kwenye jedwali la tatu la sheria ndogo hizi.

*"Mazao yanayostahimili ukame"* maana yake ni Mtama, Viazi vitamu, Muhogo na Dengu , nayo yametajwa kwenye jedwali la tatu la sheria ndogo hizi.

*"Ugonjwa"* maana yake ni maradhi ya mimea yanayosababishwa na ambukizo au kasoro na kuathiri ukuaji wa kawaida wa mimea.

*"Vitilifu"* maana yake ni wanyama, mimea jamii ya viduha, ndege na wadudu wanaoharibu mazao.

*"Viuatilifu"* maana yake ni kemikali zinazotumika kuulia au kudhibiti vitilifu.

*"Magugu"* Maana yake ni mimea yoyote isiyohitajika shambani.

*"Mkazi"* maana yake ni mtu yeyote anayeishi katika eneo chini ya mamlaka ya Halmashauri kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja lakini siyo;-

i. Mtu aliye chini ya umri wa miaka kumi na minane
ii. Mtu aliye zaidi ya umri wa miaka hamsini
iii. Mtu asiyeweza kufanya kazi kwa sababu ya ugonjwa au ulemavu
iv. Mtu aliye na kazi ya kuajiriwa ya kudumu.

Kumiliki ardhi

4 Kila mtu aliyemiliki ardhi kwa mila na jadi kwenye eneo la kanda za kilimo atalima na kutunza shamba

la mazao ya biashara na/au mazao ya chakula kwa kiasi kilichoonyeshwa kwenye safu ya nne ya jedwali la pili la sheria ndogo hizi, isipokuwa kama ataagizwa vinginevyo na Afisa mwenye mamlaka.

Utoaji wa maagizo juu ya shughuli mbalimbali za kilimo

5 (1) Halmashauri baada ya kushauriana na mamlaka nyingine za juu zinazohusika na kilimo au bila ya kushauriana na mamlaka hizo inaweza kutoa maagizo kwa maandishi juu ya aina ya kilimo, mazao ya kupanda, utumiaji wa mbolea, viuatilifu, ung'oaji wa magugu, uvunaji, na njia bora za kuhifadhi mazao.

(2) Maagizo yoyote, yatakayotolewa na Halmashauri yatachapishwa na kutangazwa katika eneo linalohusika kadiri Afisa mwenye mamlaka atakavyoona inafaa.

Kilimo cha pamba

6 (1) Kila mtu atakayelima pamba hataruhusiwa kuchanganya na mazao mengine kama vile Mahindi, Ufuta, Matikiti maji na mazao mengine kwa mujibu wa sheria ndogo hizi.

(2) Kila mtu atakayelima pamba mapema na baada ya mavuno atahakikisha anang'oa na kuchoma moto masalia yote ya pamba ifikapo tarehe 15 Septemba ya kila mwaka kwa mujibu wa sheria ndogo hizi.

Utunzaji wa mazao yaliyo shambani

7 (1) Kila mtu atakayelima shamba na kupanda mazao kwa mujibu wa sheria ndogo hizi ataliweka shamba lake katika hali ya usafi bila magugu hadi mazao hayo yatakapovunwa.

(2) Kila mtu aliyelima mazao kwa mujibu wa sheria ndogo hizi akiona mimea ya mazao yake imepatwa na magonjwa au imeshambuliwa na vitilifu atatoa taarifa haraka kwa afisa mwenye mamlaka na itambidi kutii maelekezo yote atakayopewa juu ya kuviangamiza vitilifu au mimea hiyo kwa ajili ya

kuzuia kuenea kwake.

8 Katika kukabiliana na hali ya upungufu wa chakula kila mkazi wa wilaya hii anatakiwa kulima eneo la ekari mbili za zao la Mtama au Uwele katika kila msimu wa kilimo.

Kufyeka mazao yaliyo shambani

9 Ni marufuku kufyeka au kuamuru kufekwa kwa mimea ya mazao iliyopandwa chini ya sheria ndogo hizi kwa sababu nyingine yoyote isipokuwa kwa sababu ya kuendeleza kilimo chini ya sheria ndogo hizi.

Ukaguzi wa mashamba

10 Afisa mwenye mamlaka anaweza, wakati wowote unaofaa, kuingia katika shamba lolote kwa ajili ya kukagua na kuona utekelezaji wa masharti ya sheria ndogo hizi.

Adhabu

11 Mtu yeyote atakayevunja au kushindwa kutekeleza sheria ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia adhabu yake itakuwa faini isiyozidi shillingi elfu Hamsini au kifungo kisichozidi miezi mitatu au vyote viwili, faini na kifungo.

**JEDWALI LA KWANZA**

(Sheria ndogo ya 4)

| SAFU YA KWANZA | SAFU YA PILI | SAFU YA TATU | SAFU YA NNE |
|---|---|---|---|
| *Jina la kanda* | *Jina la tarafa* | *Majina ya kata* | *Majina ya vijijji* |
| 1. Kanda ya Kaskazini | 1. Kisesa | 1. Kisesa | Kisesa, Ntobo, Ngugunu, Mwaukoli, Mwandukisesa |
| | | 2. Mwabuma | Mwabuma, Mwashata, Mwakasumbi, Baluli |
| | | 3. Mwandoya | Mwandoya, Igobe, Makomangwa, Mwakaluba, Inonelwa, Mwagumada |
| | | 4. Mwakisandu | Mwakisandu, Mwanindwa, Nyanza |
| | | 5. Mwabusalu | Mwabusalu, Nzanza, Ikigijo, Mwakipugila |
| | | 6. Lingeka | Lingeka, Masanga |
| | | 7. Mwasengela | Mwasengela, Mwabulutago, Mwamhongo, Nghanga |
| | | 8. Sakasaka | Sakasaka, Butuli, Ming'ongwa, Bulyandulu |
| | | 9. Tindabuligi | Tindabuligi, Longalonhiga, Matale, Malwilo Mnadani |
| | 2. Kimali | 10. Itinje | Itinje, Mwagayi, Mwasungura |
| | | 11. Isengwa | Isengwa, Mwageni, Mwabusungu, Semu |
| | | 12. Lubiga | Lubiga, Mwamashimba, Mbugayabanya, Mbalagane, Mwanduitinje, Isangijo |

| SAFU YA KWANZA | SAFU YA PILI | SAFU YA TATU | SAFU YA NNE |
|---|---|---|---|
| *Jina la kanda* | *Jina la tarafa* | *Majina ya kata* | *Majina ya vijijji* |
| 2. Kanda ya Kati | 2. Kimali | 1. Kimali | Paji, Sapa, Mwanyagula |
| | | 2. Mwanhuzi | Bomani, Mshikamano, Bulyanaga, Mwambegwa |
| | | 3. Nkoma | Nkoma, Mwabagalu, Ikigijo, Itaba |
| | | 4. Mwangudo | Mwangudo, Makao, Sungu, Irambandogo |
| | | 5. Mwamishali | Mwamishali, Dakama, Bulyashi, Mwambiti, Itongolyangamba, Malwilo, Mwamagingo |
| | | 6. Mwanyahina | Mwanyahina, Mwajidalala, Mwagwila, Buganza |
| 3. Kanda ya Kusini | 3. Nyalanja | 1. Mwamalole | Mwamalole, Usiulize, Lata |
| | | 2. Mwabuzo | Mwabuzo, Mwanzugi, Mwamanoni, Mwangikulu, Mwabalebi |
| | | 3. Imalaseko | Imalaseko, Nata, Mwang’humbi, Isanga |
| | | 4. Bukundi | Bukundi, Mwabagimu, Lukale, Witamhiya |
| | | 5. Ng’hoboko | Ng’hoboko, Kabondo, Isebanda, Mwafuguji, Minyanda |
| | | 6. Mwanjoro | Mwanjoro, Jinamo, Chambala, Mbushi |
| | | 7. Mwamanongu | Mwamanongu, Mwakipopo, Igushilu, Mwamagembe |
| | | 8. Mwamanimba | Mwamanimba, Mwamatiga |

**JEDWALI LA PILI**

Mazao ya biashara

| SAFU YA KWANZA | SAFU YA PILI | SAFU YA TATU |
|---|---|---|
| *Jina la Kanda* | *Mazao ya Biashara* | *Wastani wa Eneo la Shamba kwa kila Mkazi* |
| 1. Kanda ya Kaskazini | Pamba | 0.4 ya hekta (Ekari moja) |
| | Mbaazi | 0.1 ya hekta (Robo Ekari) |
| | Choroko | 0.1 ya hekta (Robo Ekari) |
| | Ufuta | 0.1 ya hekta (Robo Ekari) |
| | Dengu | 0.1 ya hekta (Robo Ekari) |
| | Alizeti | 0.1 ya hekta (Robo Ekari) |
| 2. Kanda ya Kati | Pamba | 0.4 ya hekta (Ekari moja) |
| | Choroko | 0.1 ya hekta (Robo Ekari) |
| | Ufuta | 0.1 ya hekta (Robo Ekari) |
| | Alizeti | 0.1 ya hekta (Robo Ekari) |
| 3. Kanda ya Kusini | Pamba | 0.4 ya hekta (Ekari moja) |
| | Choroko | 0.1 ya hekta (Robo Ekari) |
| | Ufuta | 0.1 ya hekta (Robo Ekari) |

**JEDWALI LA TATU**

(Sheria ndogo ya 4)

Mazao ya chakula

| SAFU YA KWANZA | SAFU YA PILI | SAFU YA TATU |
|---|---|---|
| *Jina la Kanda* | *Mazao ya Biashara* | *Wastani wa Eneo la Shamba kwa kila Mkazi* |
| 1. Kanda ya Kaskazini | Mahindi, Mtama, Uwele | 0.8 ya hekta (Ekari mbili) |
| | Mpunga | 0.1 ya hekta (Robo Ekari) |
| | Muhogo, Viazi vitamu | 0.2 ya hekta (Nusu Ekari) |
| | Karanga, Mazao jamii ya kunde | 0.1 ya hekta (Robo Ekari) |
| 2. Kanda ya Kati | Mtama, Uwele | 0.8 ya hekta (Ekari mbili) |
| | Mpunga | 0.1 ya hekta (Robo Ekari) |
| | Viazi vitamu | 0.2 ya hekta (Nusu Ekari) |
| | Karanga, Mazao jamii ya kunde | 0.1 ya hekta (Robo Ekari) |
| 3. Kanda ya Kusini | Mtama, Uwele | 0.8 ya hekta (Ekari mbili) |
| | Mpunga | 0.1 ya hekta (Robo Ekari) |
| | Viazi vitamu | 0.2 ya hekta (Nusu Ekari) |
| | Karanga, Mazao jamii ya kunde | 0.1 ya hekta (Robo Ekari) |

Muhuri Rasmi wa Halmashauri ya Wilaya ya Meatu ulibandikwa katika Sheria ndogo hizi kufuatia azimio la Halmashauri lililopitishwa kwenye mkutano wa kawaida uliofanyika Tarehe.......Mwezi.................... 2015 na muhuri huo wa Halmashauri uliwekwa mbele ya:-

Pius. Z. Machungwa

**Mwenyekiti wa Halmashauri.**

Godfrey B. Machumu

**Mkurugenzi wa Halmashauri**

**NAKUBALI,**

**Dodoma** MHE. MIZENGO K. P. PINDA (MB.),

Tarehe............Mwezi......................2015 Waziri Mkuu